Government of **Western Australia**
**North Metropolitan Health Service**
**Mental Health, Public Health and Dental Services**

# Mwongozo Rahisi: Huduma za Afya ya Meno (DHS)

Kama mtoa huduma za afya ya meno mkubwa sana katika Australia Magharibi (Western Australia) (WA) unaofadhiliwa na serikali ya jimbo, DHS inaweza kufuatilia historia yake kwa mwaka wa 1926 wakati daktari wa meno wa kwanza wa serikali alipoajiriwa na Idara ya Afya ya Umma.

## Huduma yetu

Huduma za Afya ya Meno (Dental Health Service) (DHS) hutoa huduma za meno kwa watu wa Australia Magharibi kwa kutumia mito ifuatayo za huduma.

## Huduma ya Meno ya Shule (SDS)

Huduma ya Meno ya Shule (School Dental Service) (SDS) ni mpango wa afya ya umma na hutoa huduma ya meno ya jumla bila malipo kwa wanafunzi wanaohudhuria shule ya Australia Magharibi inayotambulishwa na Idara ya Elimu ambao wana umri wa miaka 5 hadi 16 au hadi mwisho wa mwaka wa 11.

SDS hutolewa kote jimboni kupitia vituo vya meno vya eneo na vya simu (DTC) pamoja na baadhi ya shule.

Wanafunzi hutolewa na kozi ya mwanzo ya huduma wakati wa mwaka wa kwanza wa kuandikishwa na kisha wanawekwa kwenye orodha ya kusubiri ili kupokea uchunguzi wa afya tarehe ya baadaye kutegemea mahitaji yao ya kliniki. Huduma za meno za dharura hutolewa wakati zinapohitajika.

## Huduma ya Meno ya Jumla

Kliniki za meno ya jumla (General dental clinics) (GDC) hufanya kazi kote eneo la mjini na sehemu za shambani katika Australia Magharibi. Hutoa utunzaji wa meno wa jumla wa ruzuku na wa dharura kwa Waaustralia wa Magharibi wanaostahiki wa kifedha na kijiografia. Mahitaji ya ustahiki kuhudhuria GDC kwa utunzaji yanajumuisha:

- Wale ambao wanashika kadi za sasa za utunzaji wa afya au ya kibali cha pensheni na hawastahiki kwa SDS, na
- Watoto wenye umri wa miaka 0 hadi 4 ambao jina lao linaonekana kwenye Kadi ya wazazi wao ya Utunzaji wa Afya au ya Kibali cha Pensheni.

Utunzaji wa dharura unawekwa kipaumbele na hutolewa wakati unapohitajika. Wagonjwa wote wanaohitaji utunzaji wa dharura wanahitajika kupiga simu kwa kliniki ya umma ya meno ya eneo lao na kupanga miadi. Wagonjwa wanaokaguliwa kwa dharura kwa tatizo lao la meno ili DHS inaweza kuweka kipaumbele wagonjwa wenye masuala makubwa sana. Tafadhali usije kliniki bila miadi.

Orodha za kusubiri za wagonjwa wanaohitaji huduma ya meno ambayo sio dharura zinatumiwa kuhakikisha usawa wa upatikanaji kama mahitaji ya huduma zinazidi kabisa nyenzo zinazopatikana. GDC itashauri wagonjwa wakati jina lao linapofika kwenye juu ya orodha ya kusubiri. Kufuata kukamilisha kozi ya kwanza ya utunzaji, wagonjwa wanawekwa kwenye Orodha ya Kusubiri ya Kuja Tena kufanya uchunguzi wao wa afya unaofuata.

**Kuendelea kwenye ukurasa ujao**

## Huduma Maalum za Meno

Huduma ya meno ya ruzuku hutolewa kwa makundi maalum yafuatayo ya wagonjwa:

- Wakazi wanaokubali wa vituo vya utunzaji wa wazee wakazi vya mjini wanapokea uchunguzi wa meno kila mwaka bila malipo
- Wafungaji katika vituo vya Idara ya Huduma za Kurekebisha vya mjini na shambani (kawaida ni kliniki za jela)
- Watu binafsi wanaostahiki ambao wana ulemavu wa maendeleo wenye ulemavu wa akili unaohusishwa au majeraha maalum ya ubongo yaliyopatikana
- Wagonjwa wa ndani na nje ya Hospitali ya Graylands ambao wameelekezwa kutoka hosteli na hospitali zinazostahiki za magonjwa ya kiakili
- Wagonjwa wasioweza kutembea wenye mwelekezo wa kimatibabu
- Watu binafsi wanaotumia kiti cha gurudumu wenye jeraha la mgongo.

## Mipango ya Ruzuku ya Meno

DHS pia inawezesha utunzaji wa ruzuku wa meno wa kawaida na wa dhurura kwa watu wanaostahiki wa kifedha au kijiografia kupitia:

- Mpango wa Ruzuku ya Meno wa Wagonjwa wa Shambani: hulingana na utunzaji wa meno unaotolewa kupitia kliniki za meno za umma za shambani na kawaida huendesha katika mahali ambapo hana upatikanaji wa maana kwa kliniki ya meno ya serikali. Utunzaji wa meno hutolewa na wataalam wa meno wa kibinafsi wanaoidhinishwa na DHS.
- Mpango wa Ruzuku ya Meno wa Wagonjwa wa Mjini: wakati ufadhili unapowezesha, wagonjwa wanaostahiki wa mjini katika orodha ya kusubiri ya meno ya serikali wanaweza kupewa mamlaka kufanya kozi ya utunzaji wa meno usio dharura wa kawaida wa ruzuku kwa wataalam wa meno wa kibinfasi wanaoshiriki
- Mpango wa Ruzuku ya Kibinafsi ya Tiba ya Meno yaliyoota vibaya– huwezesha wagonjwa wanaostahiki wa shambani wanaowasiliana na DHS ili kupokea huduma za tiba ya meno yaliyoota vibaya za kitaalam zilizopewa ruzuku karibu nyumbani, kwa sababu huduma zote za wataalam za ruzuku zinapatikana tu sasa katika Perth.

## Ada na malipo kwa watu wazima

Malipo yote ya meno zinalingana na ratiba ya ada ya meno ya Idara ya Mambo ya Wanajeshi Waliostaafu ya serikali ya Taifa.

Ada kwa matibabu yanayotolewa katika kliniki ya meno ya umma au kliniki ya meno ya kibinafsi ya ruzuku inayoshiriki na serikali ya Australia Magharibi hadi kipeo cha 75% ya gharama ya matibabu, kutegemea mapato yao ya Centrelink. Sehemu iliyobaki ya ada ni jukumu ya mgonjwa na akaunti itatolewa. Wagonjwa wa akaunti zenye deni hawatawekwa kwenye orodha ya kusubiri au kupewa miadi kwa utunzaji usio dharura.

## Wakazi katika maeneo ya mbali

Katika maeneo ya mbali ambapo DHS ni mtoa huduma wa meno pekee, wagonjwa wote wanaweza kupata utunzaji wa meno katika kliniki ya meno ya umma. Wagonjwa wale wasiostahiki kwa utunzaji wa ruzuku wanatakiwa kulipa ada mzima.

## Kwa habari zaidi tafadhali zungumza na mtaalam wako wa meno

### Je, unataka habari zaidi au kutoa maoni?

Waraka huu unaweza kupatikana katika miundo mbadala kama vile breli, kanda la sauti au kielektronik kwa ombi.

Afisa wa Mawasiliano, Huduma ya Afya ya Meno
Locked Bag 15, Bentley Delivery Centre, WA 6983

(08) 9313 0555

publications@dental.health.wa.gov.au

www.dental.wa.gov.au

Picha zozote zinazotumiwa katika waraka huu ni kwa madhumuni ya kielelezo pekee, kwani zinatolewa tu kama mwongozo wa jumla

© 2020 Dental Health Services WA. All rights reserved.

DHS176 V 09/22_Swahili